5. **Yesu alimwaga Damu yake katika safari yake kuelekea Kalvari**

**K:** Damu Azizi ya Yesu Kristo
**W:** Sikiliza kilio cha watu wako
**W:** Tunakuabudu na kukutuza ee Krist…

6**. Yesu alimwaga Damu yake aliposulibiwa.**

**K:** Damu Azizi ya Yesu Kristo
**W:** Okoa ulimwengu na maambukizi ya korona virusi
**W:** Tukuabudu ee Kristo…

7. **Yesu alimwaga Damu yake kutoka moyo wake Mtakatifu ulipochomwa**

**K:** Damu Azizi ya Yesu Kristo
**W:** Uwe pamoja nao wanaowahudumu wagonjwa
**W:** Tunakuabudu, ee Kristo…

**K:** Waabuduo wote wameungana ulimwenguni kote kwa kipindi hiki cha shida, tusali, Baba yetu…

**Tusali Pamoja**:

Bwana Yesu, kwa imani kwa mastahili yako sasa tunachukua Damu Azizi na tunajinyunyizia wenyewe na ulimwengu mzima. Iponye wale walioambukizwa na korona virusi, utuokoe na hofu na kiburi, na mabaya, na dhambi, na magonjwa, maafa ya nguvu za asili na mlipuko wa maambukizi.


Yesu Kristo, tabibu wa wote, ubaki karibu nasi katika kipindi hiki cha mashaka na maumivu, uwe karibu na matabibu na wauguzi, wanaotafuta kuwatibu na kuwasaidia wale waliokumbwa na maambukizi ya virusi hivi. Uwe na wale wanaokufa na familia zao. Wajalie amani.

Yesu Kristo, baki nasi, tujalie amani yako na utuponye sisi na ulimwengu kupitia nguvu ya Damu Azizi. Ameni.

**Baraka\ Agizo:**

Haya maneno ya Yesu yanapatikana katika Injili ya Yohane, tumebarikiwa na kutumwa kuwa mahali pa usalama kwa wengine kupitia Damu ya Kristo: "Nawaachieni amani, amani yangu nawapa. Niwapavyo mimi Sivyo kama ulimwengu utoavyo; msifadhaike mioyoni mwenu wala msiwe na woga".

**Wimbo wa Mwisho**: *Enyi watu wote pigeni makofi*



**SALA YA ASC KIPINDI CHA MAAMBUKIZI**

**Utangulizi:**

Tupo hapa tumeungana kwa ajili ya kusali kwa ajili ya wale wameambukizwa Korona virusi, COVID 19, kwa waliofariki, kwa ajili ya familia zao na wapendwa wao. Tunawakumbuka wale wote wanaowahudumia wagonjwa kwa jinsi ya kutowajali na kuwasaidia watu waliokaribu nao wenye matatizo, wakati huo wanaendelea kuwa mbali na jamii. Tusali kwa ajili ya ulimwengu wetu, wenye fujo na machafuko, unaishi hofu, wasiwasi ukifuta faraja na Amani. Tunasali kwa matumaini kwa Majaliwa ya Mungu, anayetupatia na kutegemeza uhai hata kama hatutambui na tunaona vifo katika ulimwengu mzima. Hata Maria De Mattias anatutia moyo kwa barua yake kwa Sr. Maddalena Capone (no. 529):

Mwanangu Mpendwa katika Yesu, mimi najikuta hapa Roma ndani ya siku hizi ntafika Huko Palombara. Tujipe moyo wa shauku, na tujaze moyo ya Upendo kwa kumheshimu Mungu Mbarikiwa; tupeleke roho kwenye ubavu wa Yesu. Damu ya Yesu ni Tumaini letu lote, na ni wema wetu wote; Damu iliyomwangwa kwa maumivu na kwa upendo mkuu kwa ajili ya Uzima wetu wa milele. Tujaze moyo ujasiri bila kuogopa hata kifo kwa sababu kila wakati itukuzwe, isifiwe, ibarikiwe na kupendwa na wote!... Mwanangu mpendwa, mtumaini Mungu mkuu, na usiogope. Tujikabidhi hata kwa Maria Mtakatifu, mama yetu mpendwa na tutaona miujiza. Mungu awabariki wote watatu.
Nina haraka
Roma 19 Feb. 1853

*Kwa upendo*
*Maria De Mattias*

**Wimbo wa Mwanzo:** (wowote)

**Zab. 91**

**Somo:** Isa 26, 20 /Kut 12, 1-12

**Jibu:** Ukimya

**Somo:**

Wakati watumwa walikusanyika huko Misri usiku kuokolewa, Damu ya Mwanakondoo aliyechinjwa iliwekwa mahali salama pale walikingwa na kifo Malaika alipowaangamiza wamisri. Usiku ule wakusanyika katika nafasi hii ya uponyaji na mlo kabla ya kuondoka na kuelekea uhuru. Tunalowashwa mdomo wetu tunapokunywa Damu kwenye Kalisi (hata kama sasa haiwezekani), ni tunaweka alama kwenye miimo ya mlango wa moyo wetu kwa Damu ya Thamani. Tuseme kwamba sisi ni watu tunaopokea, wakarimu, kwamba "mwingine" anaweza kupata nafasi salama anapopendwa na kuheshimiwa… tumewekwa alama na Damu ya dal Sangue ya Mwanakondoo wa Pasaka Pasquale. Tunaitwa kuwa watu watu wanaobuni nafasi salama pale wengine wanaweza "kuwepo" katika mazingira ya kujiamini na salama.

Barry Fischer, CPPS

**SOMO:** Katiba **n. 22**

Karama ya ASC imesimikwa kwa kina katika Fumbo la kifo na Ufufuko wa Yesu. Utambulisho wetu ni wa Kipasaka, uliowekwa alama ya Damu ya Mwanakondoo. Kama Shirika tunaitwa kuachia ushuhuda wa furaha, tumaini, uwepo wetu uwe hai katika upendo unaoabudu na kukomboa wa Kristo, unaotoa maana katika mateso ya binadamu na kuwafanya huru na yenye uhai.

Tafakari ukimya mbele ya picha ya kwenye jalada kuangazia kwenye masomo ya hapo juu...

**Kushirikishana**

**Wimbo:** Wimbo wa Damu…

**Maombi:**

Sisi ni watu wenye alama ya Damu ya Mwanakondoo wa Pasaka. Tunaitwa kuwa watu wanaobuni nafasi salama pale ambapo wengine wanaweza "kuwepo" mazingira ya kuaminiana na usalama. Tusali hasa kwa ajili ya watu wanaohitaji nafasi salama Zaidi kwa wakati huu wa masahaka.

Baba yetu...

Salamu Maria...

Atukuzwe Baba….

1. **Yesu alimwaga Damu yake alipotahiriwa.**
   **K:**Damu Azizi ya Yesu Kristo
   **W:**Takasa Kanisa
   **W:**Tunakuabudu ee Kristo na tunakutukuza, kwa kuwa kwa Damu yako umeu okomboa Ulimwengu.
2. **Yesu alimwaga Damu yake katika Bustani ya mizeituni**
   **K: Damu ya Yesu Kristo**
   **W:**Iturehemu sisi na ulimwengu mzima.
   **W:** Tunakuambudu ee Kristo...
3. **Yesu alimwaga Damu yake alipopigwa mijeledi.**
   **K:** Damu Azizi ya Yesu Kristo
   **W:**Okoa roho zote zilipo toharani
   **W:**Tunakuabudu ee Kristo..
4. **Yesu alimwaga Damu yake alipovikwa taji ya miiba.**
   **K:** Damu Azizi ya Yesu Kristo
   **M:** Tusamehe dhambi zetu na utuponye.
   **W:** Tunakutukuza ee Kristo...